JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Idara ya Utumishi wa Serikali
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam.

Kumbukumbu Na. MUF 20/04/D/114

21 Septemba, 1995

# WARAKA WA WATUMISHI WA SERIKALI NA. 4 WA MWAKA 1995

## TOLEO LA PILI LA KANUNI ZA KUDUMU

1. Toleo la Kwanza la Kanuni za Kudumu (Standing Orders for Public Service) lilianza kutumika tarehe 1 Julai, 1971. Tangu wakati huo yametokea mabadiliko mengi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii hapa nchini. Aidha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali tayari zimekwishafanyiwa marekebisho yanayozingatia mabadiliko hayo. Kanuni za Kudumu nazo pia zimehuishwa ili ziweze kukidhi hali ya sasa ya uendeshaji wa shughuli za umma, mahitaji ya kazi na maslahi ya watumishi wa Serikali.

2. Mambo muhimu ya kuzingatia katika Toleo la Pili (1994) la Kanuni za Kudumu ni haya yafuatayo:—

2.1 Kanuni hizi mpya zitatumika badala ya Kanuni zilizomo katika Toleo la Kwanza la Kanuni za Kudumu.

2.2 Ikiwa baada ya tarehe 1 Machi, 1994 baadhi ya masharti yamerekebishwa kwa njia ya Waraka wa Watumishi wa Serikali, marekebisho hayo yatatumika badala ya masharti ya namna hiyo yaliyotajwa katika Toleo la Pili la Kanuni za Kudumu.

2.3 Viongozi wakuu wawe na tabia ya kusoma na kutumia kikamilifu Kanuni za Kudumu katika kutoa maamuzi yanayohusu uendeshaji kazi na maslahi ya wafanyakazi wanaowaongoza. Kwa hiyo Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea na Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa wahakikishe kuwa wanazo nakala za Kanuni za Kudumu za kuwatosha maafisa wafuatao:—

Wakuu wa Vitengo

Wakuu wa Sehemu

Wakuu wa Idara

Wakuu wa Vyuo vya Serikali

Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari za Serikali.

Wakurugenzi wa Manispaa na Wakurugenzi Watendaji wa

2.5 Kanuni za Kudumu zimepewa namba (serial number) kwenye ukurasa wa kwanza ili kurahisisha na kudhibiti utunzaji na makabidhiano yake. Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea na Wakurugenzi wa Maendeleo wa Mikoa wanapaswa kuwa na Daftari (Register) za vitabu vyao vya Kanuni za Kudumu pamoja na maingizo ya makabidhiano ya vitabu hivyo kutoka ofisa mmoja hadi mwingine.

3. Kama ilivyotahadharishwa katika Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 4 wa 1972 kuhusu Toleo la Kwanza la Kanuni za Kudumu, tahadhari inatolewa tena kuwa katika kazi yenye uzito wa namna hii, uwezekano wa kufanya makosa na usahaulifu wa mambo muhimu hauepukiki. Kwa hiyo ikiwa makosa au mambo yaliyosahauliwa yatajitokeza katika Toleo hili la Pili (1994) la Kanuni za Kudumu, taarifa iwasilishwe kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) kwa marekebisho.

CHRISTOPHER M. NYIRABU,
*Katibu Mkuu (UTUMISHI)*